# Wanawake wa Ufunuo 12

Haitakuwa ngumu kutengeneza kamusi ya kutoa maana ya ishara za unabii,kwa kuweka mafungu ya Maandiko dhidi ya  kila ishara ambapo kila ishara imetumika katika muktadha ambayo inaonyesha maana yake;ama katika maelezo ya kihistoria,maadhimisho ya sikukuu,au sheria zilizotungwa ili kuleta mwanga juu yake. Kuchunguza Maandiko,ni kupata suluhisho ya maneno magumu katika kitabu hiki,kwa sababu kimehusiana sana na Biblia nzima jinzi inavyoonekana na msomaji wa juu juu.

Hata hivyo,twaendelea kuchunguza kwa ufupi unabii unaoongoza wa *Ufunuo*,ufahamu ambao watosha kutambua upeo na hulka zake.Ni aina mbili za baadhi ya ishara muhimu katika mifuatano mizima, zinachukua sura nzima,na kama imedokezwa kwa wengine; zinahusiana kwa kila moja, na kwazo zimefafanuliwa kiroho. Hii ni njozi ya BABELI MKUU,katika ***sura ya kumi na saba*** ya kitabu,unabii ambao kwa upatanishaji wake na tabiri nyingine za Ufunuo,unaleta dokezo   ya thamani kwa maana yake na matumizi ya mfuatano mzima ya njozi. Unabii huu pia una umuhimu wa vitendo, unaoufanya uwe na maana ya kipekee.

Mara kabla ya kuanguka kwa Babeli, kulikoelezwa katika ***sura ya 18*** ya Ufunuo,sauti kutoka mbinguni inasema, “ Tokeni kwake,enyi watu wangu,msishiriki dhambi zake, wala msipokee mapigo yake. Kwa maana dhambi zake zimefika hata mbinguni,na Mungu amekumbuka maovu yake.” Je! Si muhimu kwamba Wakristo wanapaswa kuwa wazi kwa mfumo ambao sauti kutoka mbinguni ya  taadhima inakemea?Na pia,baada ya kuanguka kwa Babeli, “sauti kuu kama ya watu mbinguni,” inasikika ikisema,kwa kurejelea hiyo, “Haleluya,Wokovu,na utukufu na nguvu,zina Bwana Mungu wetu;kwa kuwa hukumu zake ni za kweli na za haki;maana amemhukumu yule kahaba mkuu aliyeiharibu nchi na uasherati wake,na kuipatiliza damu ya watumwa wake mkononi mwake.Wakasema mara ya pili,Haleluya.Na moshi wake hupaa juu hata milele na milele.”…

Ukengeufu  unaonekana kwa “Babeli Mkuu,” kusihi kwa njia ya kipekee kwa watu wa Mungu watoke kwake,na uharibifu mkubwa na kushangaza ulionenwa dhidi yake,zote zimewekwa pamoja kuleta umuhimu wa kupata *kujua makusudi ya mfumo huu hasa*?

Tukichunguza sura ya **17 na 18** ya Kitabu cha Ufunuo zinaonyesha kwamba “Babeli Mkuu” unaonyesha mfumo ambao unapaswa kudumu kwa muda mrefu,na kuwa na ushawishi mpana,na utakuwa na hatia ya kuzidi kufanya maovu na ukatili.Huu mfumo lazima uwepo,ambapo uharibifu wake utatokea polepole wakati wa “harusi ya Mwana Kondoo,” na ni tukio ambalo twajua kwamba ni la usoni;na twaona pia kwamba hadi wakati wa uharibifu wake,ama karibia wakati huo,watoto wa Mungu watapatikana kuwa mbali naye,ili kwamba kutakuwa na mahitaji ya mwito wa dharura, “*Tokeni kwake,enyi watu wangu*.”

Mfumo huu umeonekana kama mkatili unaotesa,kama mfumo ambao “ amelewa kwa damu ya

watakatifu ,na kwa damu ya mashahidi wa Yesu," yule ambaye Bwana Mungu "atalipatiliza damu ya watumwa wake." Bwana Yesu Kristo,ambaye anapenda Kanisa lake alipoona uwepo na kazi ya mfumo huu mbaya,alitoa onyo,na kuonya huyo mwanamke kwa unabii.Anamwekea alama nyingi ambapo kahaba anaweza kutambulika kwayo.na anamwonya kwa upole dhidi ya kufanya vita ama ulegevu,wakati anamhamasisha na kumhimiza kwa migogoro na mtazamo wa matokeo ya mwisho.Angeweka watu wake kwa utatanishi na shaka kwa swali kuu,kwa hiyo ametabiri kwa hali ya kipekee;ameiweka kwa hali iliyochorwa na kwa ulinganifu wa kukusudia na unabii mwingine,ambao unafanya maana yake wazi sana,na pia ameongeza pia maelezo ambayo yanaacha nafasi ya mwanafunzi wa kweli kufanya kosa.

Wacha msomaji atazame vipengele tofauti vya ishara za kubainisha:

**"Kahaba Aketiye Juu ya Maji Mengi."**
**"Babeli Mkuu."**

"Akaja mmoja wa wale malaika saba,mwenye vile vitasa saba,akanena nami,akisema,Njoo huku,nitakuonyesha hukumu ya yule KAHABA MKUU aketiye juu ya maji mengi.

"Akanichukua katika Roho hata jangwani,nikaona mwanamke,ameketi juu ya mnyama mwekundu sana,mwenye kujaa majina ya makufuru,mwenye vichwa saba na pembe kumi.

"Na mwanamke yule alikuwa amevikwa nguo ya rangi ya zambarau,na nyekundu,amepambwa kwa dhahabu,na kito cha thamani, na lulu,naye alikuwa na kikombe cha dhahabu mkononi mwake,kilichojawa na machukizo,na machafu ya uasherati wake.Na katika kipaji cha uso wake alikuwa na jina limeandikwa,la siri,BABELI KUU,MAMA WA MAKAHABA NA MACHUKIZO YA NCHI.

"Nikamwona yule mwanamke amelewa kwa damu ya watakatifu,na kwa damu ya mashahidi wa Yesu" (***Ufu. 17:1-6***).

**"Bi Harusi,Mke wa Mwana Kondoo."**
**"Yerusalemu Mpya."**

"Akaja mmoja wa wale malaika saba waliokuwa na vile vitasa saba vilivyojaa yale mapigo saba ya mwisho,naye akanena nami ,akisema,Njoo huku,nami nitakuonyesha yule BIBI-ARUSI,mke wa Mwanakondoo.

"Akanichukua katika Roho mpaka mlima mkubwa, mrefu, akanionyesha ule mji mtakatifu Yerusalemu, ukishuka kutoka mbinguni" (Bibi-arusi, Mke wa Mwana Kondoo,akiwa chini ya ishara nyingine) (***Ufu.. 21***).

"Naye amepewa kuvikwa kitani nzuri, ing'arayo,safi kwa maana kitani nzuri hiyo ni matendo ya haki ya watakatifu" (***Ufu. 19:8***).

Bibi Harusi ameelezwa kama “YERUSALEMU MTAKATIFU ambao unashuka kutoka mbinguni kwa Mungu,ukiwa na utukufu wa Mungu;na mwanga wake ni kama jiwe la thamani" (***Ufunuo 21***).

Joka “alimwudhi mwanamke,” na “akamkasirikia yule akaenda zake afanye vita juu ya wazao wake waliosalia, wazishikao amri za Mungu,na kuwa na ushuhuda wa Yesu Kristo" (***Ufu. 12:13-17***).

Kuhusu Babeli,Yohana anaongeza kwa kusema, “ nami nilipomwona nikastaajabu ajabu kuu.Na yule malaika akaniambia,Kwani kustaajabu? Nitakuambia siri ya mwanamke huyu,...Vile vichwa saba ni milima  saba anayokalia mwanamke huyo.Yale maji uliyoyaona,hapo aketipo yule kahaba,ni jamaa na makutano na mataifa na lugha…Na yule mwanamke uliyemwona ,ni mji ule mkubwa,mwenye ufalme juu ya wafalme wa nchi. (***Ufu. 17:7***).

Unabii huu unaonyesha kwa upana wanawake wawili waliotofautiana,ametambulika na miji miwili tofauti,hakika ya kila mmojawapo,wote wanaonyeshwa kama mwanamke,na pia kama mji.Kahaba na Babeli ni moja;Bibi arusi na Yerusalemu wa mbinguni ni mmoja.

Ni hakika kwamba ufafanuzi wa kweli wa maonyesho haya mawili lazima yatoe dokezo la maelezo ya kweli kwa nyingine.

Wanawake wawili hawa wametofautiana katika kila jambo ambalo linanenwa kuwahusu;mmoja ni halisi kama usafi mwenyewe, “amejiweka tayari” na ametosha kwa utakatifu wa mbinguni;mwingine,ni mchafu kwa ajili ya ufisadi wake,na yuatosha moto wa uharibifu.

Mmoja ni wa Mwana Kondoo,ambaye amempenda kama vile Bwana arusi yuampenda Bibi arusi,mwingine anahusiana na mnyama wa pori,na wafalme wa dunia,ambao baadaye watamchukia na kumharibu.

Mmoja amevikwa na kitani safi—haki;wakati mwingine amevikwa katika rangi nyekundu na dhahabu,na kito cha thamani na lulu,kwa kweli ameng’aa,lakini kwa mapambo ya kidunia pekee.

Mmoja ameonyeshwa kama bikra safi aliyeposwa na Kristo; mwingine ni mama wa makahaba na machukizo ya dunia.

Mmoja aliteswa,akafinywa sana na Joka,na kukimbizwa nyikani,na likakaribia kulemewa;mwingine amelevya kwa mvinyo wa damu ya watakatifu,na *amekaa* juu ya mnyama ambaye amepokea nguvu kutoka kwa nyoka ateswaye.

Mmoja anaishi kwa hali ya upweke nyikani, mwingine “anatawala nyikani” juu ya mataifa,na watu na lugha.

Mmoja anaandamana pamoja na Mwana Kondoo kwa mamkuli ya harusi,huku kukiwa na shangwe na haleluya ya mbinguni;mwingine amechapwa,kuraruliwa,na kuharibiwa,na kosa la hawara wake.

Tunapoteza mtazamo wa Bibi harusi huku kukiwa na mnga'ro wa utukufu wa mbinguni na furaha,na kwa kahaba kukawa na viza na giza ya moshi ambao " unainuka juu milele na milele."

Ni vigumu kupata katika Maandiko tofauti iliyowekewa alama;na hitimisho ambayo haiwezi kupingwa,kwamba kwa kile ambacho mtu anaonyesha,lazima kingine kionyeshe *kinyume*.Siyo maoni ambayo yamekosa kushikana,lakini kila mmoja yashikana,siyo kwa kufanana,lakini kwa ulinganifu.

Basi,Maandiko yanatuacha bila shaka kuhusu umuhimu wa ishara ya Bibi Harusi,Mke wa Mwana Kondoo,ambaye ni Yerusalemu wa mbinguni.Twasoma, " Enyi waume,wapendeni wake zenu,kama Kristo naye alivyolipenda Kanisa,akajitoa kwa ajili yake;ili makusudi alitakase na kulisafisha kwa maji katika neno apate kujiletea Kanisa tukufu,lisilo na ila wala kunyanzi wala lo lote kama hayo;bali liwe takatifu lisilo na mawaa." " Kwa kuwa tu viungo vya mwili wake." Kusudi la upendo wa Kristo,kulingana na damu yake-lilinunua kanisa ni kwamba anapaswa kuishi naye,na kuwa naye milele;ili kwamba amtazame na kumshirikisha katika utukufu wake,akimbadilisha katika mfano wake.Hapa,katika maono ya unabii,twaona muundo uliobarikiwa ukikamilishwa,na kanisa lililokamilishwa na kuwekwa wakfu kikamilifu,liliovalishwa kanzu ya haki,na kuletwa kwa karamu ya Mwana Kondoo.Twaona akiteswa kama Bwana wake,na ameteswa pamoja na Bwana wake na pia wakatukuzwa pamoja.Zaidi ya maswali yote,Bibi harusi wa Yerusalemu mpya anawakilisha *kanisa la kweli la Kristo.*

Je! Ishara hii ya ulinganifu wa kahaba wa Babeli inaonyesha nini? Kwa kweli ni kanisa la uongo na kanisa lililoasi,kanisa ambalo linakiri kwamba ni la Kristo,lakini limejitoa kushiriki na ulimwengu,na limeshikana kwa karibu sana na wafalme wa dunia;kanisa la kiulimwengu,ambalo limeacha upendo wake wa kwanza,na kusahau mwito wake wa mbinguni,na kujizika ndani ya nia ya binadamu na dhambi,na kuhakikisha kuwa la aibu na kukosa uaminifu kwa Bwana wake.

Utazamwe kwamba ishara hizi,mwanamke na mji,zinaonyesha mifumo dhahiri,miili ya ushirika,siyo tu watu wanaofanana lakini wanaotengana.Magugu yaliyoko katika konde la ngano,samaki mbaya ndani ya wavu,huonyesha huyu;lakini hapa hatuna Mkristo wa kweli wala maprofesa wa ulimwengu,ni kama mtu binafsi lakini mashirika wawili,miili miwili dhahiri.Kanisa la kweli la Kristo ni mwili;washirika wake wameungana pamoja katika umoja na Kichwa chao na kushikana pamoja,uhai mmoja unawahuisha: "Kwa sababu naishi,nanyi pia mtaishi;" roho moja hukaa ndani yao,ni maskani moja ya Mungu.kiungo ambacho kinawashikanisha,hata hivyo,cha kiroho,ambacho ni mwili unaoonekana.Kanisa la uongo haliwezi kuwa na kiungo hicho.Kifungo kinachowapatanisha lazima kiwe kibaya,cha nje,kinachoonekana;kanisa linalowakilisha Babeli lazima liwe kanisa lionekanalo,shirika la kidunia,na laweza kutambulika na kujulikana….Mwanamke na mji moja-ikiwa twaweza kupata

jina la mji,basi tutaweza kutambua kanisa likusudiwalo.

Neno la mwisho la Yohana halikuonekana kuacha uwezekano wa kosa kulingana na mji. “Vile vichwa saba ni milima saba anayokalia mwanamke huyo….Na yule mwanamke uliyemwona,ni mji ule mkubwa,mwenye ufalme juu ya wafalme wa nchi.” Ni mji gani huo? Kulikuwako na mji mkubwa ambao kwa nyakati za Yohana,ulitawala juu ya wafalme wa dunia.Ulikuwa mji wa Rumi.Na Rumi ulikuwa mji mkubwa wakati huo,na umekuwa mkuu-kwa njia hii au nyingine tangia wakati huo hadi leo hii.Na Rumi ulikuwa juu ya milima saba—“milima saba anayokalia mwanamke.” Jina lake la kawaida kwa wale waandishi waliobobea wa awamu ya Mt.Yohana ni “mji upatikanao juu ya milima saba;” sikukuu ya kila mwaka unaosherehekewa kwa ajili ya “ mji wa milima saba” inakaririwa na mtunga shairi wa Kilatini,kwa muda wa miaka mia tano linaonyesha milima saba ya Rumi.Medali na sarafu ya siku hiyo zinaonyesha Rumi kama mwanamke aliyekaa juu ya milima saba;na majina yake yaonyesha,kwa wazi jinsi alitawala kabisa.Alipewa jina “Rumi wa kifalme;” “Bimkubwa wa ulimwengu;” “malkia wa mataifa.” Alikuwa na ushawishi wa ulimwengu mzima.Alikuwa jiji kubwa wa utawala wa nne ambao Danieli alitabiri kwamba utavunjika vipande vipande na kuangamiza kila kitu, “wa kutisha na mbaya na mwenye nguvu nyingi;” na kwa wakati wa maono ya Ufunuo,nguvu zake zilikuwa kileleni.Rumi na sio mji mwingine,ndio unarejelewa hapa;mwanamke huyu anatambulika kama Rumi.Tuliona hapo awali kwamba lazima awakilishe kanisa,sasa twajua ni kanisa gani.Kahaba ni Kanisa la Rumi;kwa watu wenye fikra nyepesi inaonekana kwamba hakuna kuepa hitimisho hili.” Mwanamke uliyemwona ni mji mkubwa” “ mwenye ufalme juu ya wafalme wa nchi.”

Swali ambalo kwa kawaida linapendekezwa lenyewe ni,Ikiwa mwanamke huyu amatambulika kwa njia nyingine na RUMI,kwa nini paji la uso wake limeandikwa jina BABELI? Jibu ni wazi,Ufunuo ni Kitabu cha siri;vitu vinaonyeshwa kwa ishara;kweli zinafunuliwa;na ingekuwa kinyume na mtindo mzima wa unabii huu wote kama RUMI ungeandikwa kwa uso la kahaba.Mwanamke ni umbo la kanisa,kanisa la ufisadi na la kuabudu sanamu,yaani ishara Yohana aliona ilionyesha kitu kilicho tofauti kwa kilichokusudiwa,hata hivyo kilikuwa sawa kiajabu.Kahaba ni “Siri,Babeli Mkuu.”

Majina yalikuwa yanapeanwa kama maelezo ya tabia au kazi; kwa mfano, Mariamu aliambiwa amwite mtoto wake Yesu, ambalo lilimaanisha *mwokozi*,kwa sababu *alipaswa kuokoa watu* wake kutoka kwa dhambi zao.Jina Babeli,linatumika na Roho kwa Kanisa la Rumi,linaashiria tabia ya Babeli kwa sababu Babeli lina maana ya mchanganyiko—machafuko (*tazama Walawi 18:23*).Huu muungano wa mwanamke (kanisa) na mnyama (utawala) unaunda ukahaba wa kiroho ambao amekuwa nao na hatia.
Lakini (Babeli) linawakilisha familia nzima;binti zake ambao wamemiliki jina lake na asili yake,kwa sababu ni “*mama* wa makahaba,” na kazi zake pia wanazifanya.Binti zake wengine wamefuata nyayo zake kwa karibu sana,kwa kuchanganya Kanisa na Serikali.Hao ni kama “Kanisa la Kianglikana” na makanisa mengine ya kiserikali.Na binti wengine pia watakuwa hivyo wakipata utawala mbao unawasaidia.

Roho ile ya *machafuko*—Kanisa kutembea na muungano ulioasi wa ulimwengu—inaonekana

kwa kila njia.Kanisa( la kawaida) na ulimwengu wanatembea sako kwa bako na ulimwengu,wanaungana pamoja na kusherehekea pamoja.Ni kipengele cha ulimwengu na mali yake ndiyo yanatafutwa na kila dhehebu kusaidia Kanisa katika kiwango cha kifahari wanachotaka kufurahia.Ndiyo maana si ajabu kwetu tukiona makanisa ya Kiprotestani wakilegea kwa maadili ya Mungu na kuruhusu ushoga na mambo mengine,wale ambao wanaketi katika sinagogi,wale wanaolisha kundi.Ole, jina Babeli limeandikwa katika paji la uso wa kila mfumo wa kidini upatikanao ulimwengu mzima! Japo wote,kama mfumo wa mama,wanashikilia " kikombe cha dhahabu ( Neno la Mungu) linalojaa machukizo ya (Kiyunani,*kai*) na machafu ya ukahaba wake," bila kuona haya kwa aibu yake,na hakika kwamba hawafahamu ukweli kwamba inawahukumu.

Lakini kikombe cha hasira ya Mungu kimejaa.Mungu hatakuwa na subira na huruma tena,na japo hadi wakati wa mavuno,aliruhusu ngano na magugu kukua pamoja,amri muhimu sasa ni, "Tokeni kwake,enyi *watu wangu*." Sumaku ya ukweli inasanya vito,na aibu za ulimwengu na Kanisa la kawaida wanasafisha na kuwaweka kwa matumizi ya Bwana.

Yeye basi hutafuta "kundi dogo"—Kanisa la kweli—ambalo jina lake limeandikwa mbinguni, ambaye alikuwa akingojea kurudi kwake hata kama hakuwepo, walichunguza kwa makini kila andiko lake ambalo lingewafahamisha kurudi kwake na utukufu,na mapenzi yake yaliyowahusu;wale waliofanya na kutoa dhabihu ya mvuto wa kidunia,ili wapate raha idumuyo na heshima kuliko heshima yote ulimwengu unaweza kutoa.Ndiyo, "Watakuwa wangu,asema Bwana,siku hiyo ambayo natengeneza vito vyangu." (***Mal. 3:16,17***).

Koreshi aliyetawala Babeli,na kuwacha huru Waisraeli wa kimwili toka kwa utumwa ni kama aina ya Kristo.Katika kuwacha aina,sio kwamba mji mkuu (Babeli) ulitupwa peke yake lakini utawala wote na mikoa na miji yake yote.Kwa hivyo mji wa Babeli huu ,na sio mji mkuu peke yake—makao makuu na mfumo wa Kanisa lililoasi (Kanisa la Rumi)—lakini yote chini ya utawala wa ulimwengu-machanganyiko yote,machafuko yote---mama na binti zake.

Babeli ndio utaanguka na kusiagwa vipande vipande katika siku ya Bwana,lakini bikra wa kweli na mwaminifu atakusanywa na kufanywa kamilifu,na kama Bi harusi na warithi sawasawa naye,watashiriki katika utukufu wa Kristo

"Mpendwa hili ni Kanisa la Mungu,
Kuta zilizo mbele zake zimesimama;
Zapendeza kama mboni ya jicho lake,
Na kuchongwa kwa mkono wake."

Henry Grattan Guinness R471

---